# MAOMBI



## Ya Hemani

BY DENIS & DEVIS JULIUS

**UTANGULIZI:**

Ni rahisi mtakatifu kukesha kuomba, lakini kuomba kwa usahihi si wengi wetu tunafahamu. Hivyo katika makala hizi, ambazo zipo katika mfululizo utajifunza mambo muhimu ambayo unapaswa ujifunze kuyaomba kwa Mungu kwa faida ya ukuaji wako kiroho.

Maombi ni mahusiano, yaani ni mazungumzo kati ya mtu na Mungu, hivyo Mungu ameweka utaratibu wake tunakwenda kusema naye, Na ndio maana ametupa Roho wake Mtakatifu kutusaidia kujua jinsi ya kuomba kama atakavyo yeye.

Katika makala hii, tutaona ni jinsi gani makuhani waliwasilisha maombi yao kwa Mungu ndani ya hema, na hivyo kama walivyofanyika kivuli cha agano jipya tutaona na sisi tunawasilishaje yetu kwake.

Mwongozo huu, ni wa maombi yako binafsi ya siku. Ambayo utaomba si chini ya dakika 100, yaani (saa 1:40). Uwapo mahali pako pa sirini na Mungu. Kila mwisho wa kipengele tumeweka dakika unazopaswa kuombea katika eneo hilo.

Lakini pia ukuaji wa kiroho hutegemea usomaji wa Neno la Mungu. Hivyo basi katika tovuti yetu hii www.wingulamashahidi.org. Utakutana na mafundisho mengi, pamoja na majibu ya maswali wengi ya biblia zaidi ya 4,000. Tembelea utajifunza mengi.


**Zingatia:** Omba katika mazingira ya utulivu wa roho, elekeza mawazo yako kwa Bwana, na kwa jinsi utakavyokuwa unatamka vipengele hivyo, huko huko Kristo naye atakupa kinywa cha maombi utaomba hata zaidi ya hivyo tulivyoviorodhesha, utamfurahia Mungu sana.

Bwana akubariki.

Karibu sasa katika mwongozo wetu..

~Mwl Denis & Devis Julius

# MAOMBI YA HEMANI.



Waebrania 4:15 Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. 16 ***Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.***

Katika maombi yetu tumeambiwa tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri tupate rehema. Lakini si wote wanafahamu kiti cha rehema Kipo wapi? Na tunakifikiaje. Tunachofahamu ni kusema “ninakikaribia kiti cha rehema, Bwana nisaidie hiki na hiki”. Ukweli ni kwamba kila mahali pana utaratibu wake, huwezi ingia tu ghafla chumbani mwa baba yako, bila kubisha hodi, hata kama ni Baba yako mzazi upo naye nyumba moja ambaye una haki ya kumweleza matatizo yako wakati wowote. Halikadhalika, tulipoambiwa tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri haimaanishi tusiende kwa utaratibu. Ndio hapo mwamini, inakuwa shida kwake, kufurahia maombi, au wakati mwingine kutojibiwa kwasababu tu hazingatii kanuni za Mungu.

Hivyo mwongozo huu utakusaidia, kuelewa kwa undani, maombi yetu kama makuhani tunayawasilisha vipi kwa Mungu mbele ya kiti cha rehema, sawasawa na makuhani wa Mungu walivyofanya katika agano la kale.

Katika ile hema ya kukutania, ambayo Mungu alimwagiza Musa aitengeneze, akutane na watu wake kuzungumza nao. Ilikuwa imegawanyika katika sehemu kuu tatu, (Kutoka 25-27)

1. Ua wa nje
2. Patakatifu
3. Patakatifu pa Patakatifu

**Katika ua wa nje, kulikuwa ni vitu viwili.**

i. Madhabahu ya shaba ya sadaka za kuteketezwa
ii. Birika la shaba la kunawia

**Ndani ya hema, yaani "patakatifu" palikuwa na vitu vitatu.**

i. Meza ya mikate ya wonyesho
ii. Kinara cha taa cha dhahabu
iii. Madhabahu ya dhahabu ya kuvukizia uvumba

**Ndani ya hema nyuma ya pazia  yaani, "patakatifu pa patakatifu" kulikuwa na**

**i.** Sanduku la agano: Ambalo ndani yake kulikuwa ni fimbo ya Haruni, Mana, na Vibao viwili vya amri kumi. Na juu ya yake ndipo kilipokuwepo kile **"KITI CHA REHEMA".**

Hivyo  kuhani mkuu alipotaka kukifikia kiti cha rehemu. Kulikuwa na taratibu zake. Ni lazima ukutane vitu hivi sita, kama ifuatavyo.

### 1. MADHABAHU YA SHABA YA SADAKA ZA KUTEKETEZWA



Sadaka ilipoletwa, na kuchinjwa, iliteketezwa pale nje, katika hiyo madhabahu iliyojulikana kama madhahabu ya shaba ya sadaka za kuteketezwa, ilichomwa yote. Lakini damu yake huchukuliwa na kuhani, kuingizwa ndani.

*Ufunuo wake kwa agano jipya ni upi?*

Sasa na wewe kama mwombaji, lazima uitambue sadaka yako, ambayo huna budi kuileta madhabahuni pa Mungu, uichome mpaka iteketee kabisa, kabla ya kupiga hatua ya kukikaribia kiti cha rehema kule ndani. Na sadaka yetu sisi sio fedha, au mazao, bali ni YESU KRISTO.

Yeye ndio mwanakondoo aliyechinjwa kwa ajili yetu, Hivyo na wewe huna budi kumchinja Kristo hapo, na kumteketeza kabisa, Sasa tunamchinjaje? Ni sisi kutambua na kukiri kazi ya Kristo ya ukombozi iliyokamilika pale msalabani.

Hivyo ili rohoni uonekane umemchinja rohoni unapaswa utafakari na ukiri mambo makuu ya manne (4),

- **Kwa kupigwa kwake, umepokea msamaha wa dhambi (Wakolosai 1:12-14).** ~Dk 10

Hapa unatambua kuwa sio kwa matendo yako umepokea wokovu na msamaha wa dhambi, bali kwa neema yake, Unasema, Asante Bwana kwa kuwa mimi sihesabiwi dhambi na wewe, Kwasababu wewe tayari ulifanyika kuwa dhambi kwa ajili yangu. Hapa tumia muda wa kutosha kumshukuru Kristo kwa neema yake ya ajabu.

- **Kwa kupigwa kwake umeponywa. (Mathayo 8:17, 1Petro 2:20).** ~Dk 10

Hapa unakiri uzima, Mungu aliokupa kwa kifo chake msalabani. Kwamba huna ugonjwa, wala udhaifu, wala upungufu wowote katika mwili wako wala roho yako, kwasababu yeye tayari alishayachukua masikitiko yetu, na magonjwa na huzuni zetu. Unakiri hivyo kwa muda wa kutosha mpaka uone amani ya kuendelea eneo lingine.

- **Kwa kupigwa kwake umebarikiwa (umekuwa tajiri)** 2Wakorintho 8:9 ~Dk 10

Vifungu hivyo vinasema alifanyika maskini ili sisi tuwe matajiri. Lazima uukiri utajiri wa Kristo. Na utajiri ni uwezo wa kuyafikia maono yako. Hivyo wewe si maskini ndani ya Kristo. Hilo unalikiri kwa kumtafakari Kristo aliyeacha enzi na mamlaka akawa maskini ili mimi na wewe tuwe matajiri, muda huu unaukataa umaskini kwa imani.

- **Kwa kupigwa kwake umefanywa huru(Mbali na vifungo). Luka 4:18** ~Dk 10

Kifo cha Yesu msalabani, ilikuwa pia ni ili sisi tuwe huru, mbali na laana zote, za yule mwovu. Ndio maana siku ile alipokufa makaburi yakapasuka, wafu wakafufuliwa. Vivyo hivyo na wewe upo huru mbali na vifungo na laana zote, za ukoo, za kimila, za kifamilia,

za kipepo n.k. Hakikisha unakiri hivyo kwa imani kwa muda wa kutosha, Na ndivyo unavyothibitisha uzima wako kwake.

## 2. BIRIKA LA SHABA.




Kama tulivyoona birika, hili liliwekwa mlangoni mwa hema ambapo makuhani walinawa mikono na miguu yao, kabla ya kuingia ndani. Hivyo iliwapaswa waingiapo ndani, basi mikono yao na miguu yao iwe safi kabisa.

*Hili hufunua nini kwa agano jipya?*

Kunawa miguu: Ni unyenyekevu wetu sisi kwa sisi. Utakumbuka wakati ule Bwana kabla hajasulubiwa, aliwaketisha wanafunzi wake akaanza kuwatawadha miguu (Soma Yohana 13:12-19). Alipomaliza akawaambia ikiwa mimi niliye Bwana wenu, nawatawadha ninyi miguu, imewapasa ninyi kwa ninyi mtawazane miguu. Akiwa na maana tunapaswa, tunyenyekeane.

- **Hivyo kabla ya kukikaribia kiti cha rehema, jichunguze Je! Kiburi kwa wenzako kipo ndani yako**?. Kama ni ndio hapo hapo iponye roho yako, kwa kujishusha kwa kumaanisha kugeuka. ~Dk 5
- **Pia safisha mikono yako kwa kuachilia, kusamehe, kupatana na ndugu yako,** kumpenda Ndugu yako. Bwana alisema pia maneno haya katika; ~Dk 5

*Mathayo 5:23  Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, 24  iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako.*

Usitoe sadaka ikiwa mikono yako ni michafu. Patana na ndugu zako, kisha mtolee Bwana.

Hivyo kunawa miguu na mkono, ni kujinyenyekeza na kukumbuka unapaswa umpende ndugu yako kama nafsi yako. Tengeneza hapo kwa dakika za kutosha mpaka uone amani imeingia moyoni mwako, hakuna kikwazo.

## 3. MEZA YA MIKATE YA WONYESHO.

---



Meza hii, ilikuwa ndani ya hema, upande wa kuume, ambapo juu yake kuliwekwa mikate 12, ambayo ilikuwa inabadilishwa kila wiki. Makuhani tu ndio walioruhusiwa kuila.

*Katika agano jipya hufunua nini?*

- **Kabla hujakaribia kiti cha Rehema fahamu una wajibu wa kula mkate wako wa uzima. Na huo si mwingine zaidi ya Neno la Mungu**. Mungu anatarajia sana wewe kama mwombaji ujawe na Neno la Mungu ndani yako, kabla ya kukikaribia kiti cha rehema. Je! Una Neno la kutosha ndani yako. Tumia dakika za kutosha tafakari Neno la Mungu, tangu mwanzo mpaka ufunuo, Pia ni lazima ujiwekee desturi ya kuisoma biblia walau sura kadhaa kila siku, husasani kabla hujaiongia kwenye maombi. Utaonekana ni kuhani ambaye hajapungukiwa Neno la Mungu ndani yake. Wakati wote mikate ipo. ~Dk 15

*Wakolosai 3:16 Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*

## 4. KINARA CHA TAA CHA DHAHABU



Kinara hichi, kiliwekwa upande wa kushoto mwa hema, kilikuwa na mirija saba, na yote ilipaswa iwake bila kuzima daima, kwasababu mwanga wa kinara kile ndio uliomulikisha hema zima. Pasipo kile ndani ni giza.

<u>*Katika agano jipya ilifunua nini?*</u>

- **Roho saba za Mungu:** ~Dk 30

*Ufunuo 4:5 Na katika kile kiti cha enzi kunatoka umeme na sauti na ngurumo. Na taa saba za moto zilikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi*, *ndizo Roho saba za Mungu.*

Hivyo wewe kama mwombaji huna budi kuomba Roho Hizi saba za Mungu ziwake ndani yako daima. Na hizo ndio tunazisoma katika;

Isaya 11:1-2

"*1 Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda. 2 Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana"*

Unaanza sasa kuomba Roho moja baada ya nyingine, ijae ndani yako, kuanzia ile Roho ya Bwana,iliyokuwa juu yake ya upendo ya kujitoa sadaka kwa ajili ya wengine, kisha ya hekima mfano wa iliyokuwa juu ya Sulemani, kisha ufahamu, kisha ya shauri , kisha ya uweza (yaani nguvu) kama Eliya, kisha ya maarifa kama

iliyokuwa juu ya Danieli,  na ile ya kumcha Bwana kama Ayubu. Zote hizo zijawe ndani yako.

- Ni muhimu sana, hapa ndio kiini cha maombi yako kinapaswa kiegemee. Kwasababu katika Roho hizi zote, basi mambo mengine yote yamo ndani yake. Hivyo omba hizi Roho saba kwa muda mrefu, huku ukirejea mifano ya watu waliokuwa na Roho hizo kwenye biblia.

## 5. MADHABAHU YA DHAHABU YA KUVUKIZA UVUMBA



Hii ndio ile kuhani huenda na manukato kisha huyachoma juu ya madhabahu ile katika chetezo chake, na moshi wa manukato yale, hufunika hema yote na kupaa juu.

*Hufunua nini kwa agano jipya?*

- **Nyimbo za sifa.** ~Dk 15

*Ufunuo 5:8  Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya*

*watakatifu. 5.9* ***Nao waimba wimbo mpya*** *wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa,*

Tumia muda wako wa kutosha kumsifu Mungu na kumwimbia katika hatua hii. Ni muhimu sana. Sifa tu zenyewe ni aina mojawapo ya maombi ya mwamini.

## 6. <u>SANDUKU LA AGANO</u>



Sanduku hili lipo nyuma ya pazia, ambapo panajulikana kama patakatifu pa patakatifu. Ndani ya sanduku hili kulikuwa na ile fimbo ya Haruni, mbao mbili za amri kumi, pamoja na ile mana. Lakini kwa juu yake ndipo kulikuwa na kile kiti cha Rehema, ambapo kuhani mkuu huinyunyiza damu juu yake. Kisha upatanisho unapokelewa.

*<u>Hufunua nini katika agano jipya.</u>*

- **Kabla ya kukifikia kiti cha rehema, lazima ujue ndani yake zipo amri za Mungu ambazo zinapaswa zishikwe, hivyo uombapo, tafakari amri moja baada ya nyingine je, umezishika, kama la! Unaomba Roho akusaidie**, kuziishi tangu huo wakati, vilevile lazima uombe Bwana akupe ufunuo wa Neno lake (Ndio mana iliyofichwa) Ufunuo 2:17, lakini pia utambue ipo fimbo ya kichungaji ya Yesu iwaokoayo wanadamu, mwambie Bwana siku zote uitazame ikufariji kama Daudi alivyoomba kwa Mungu katika (Zaburi 23). ~Dk 5

- Baada ya hapo sasa ndipo unakikabili kiti cha rehema, ukitambua kuwa ni kwa damu ya YESU, unasikiwa maombi yako. **Hapo ndipo sasa, umwambie Bwana mahitaji yako yote ambayo unatamani akutendee.** Kwasababu umezingatia kukikaribia kiti cha Rehema kwa utaratibu Mungu anaouhitaji. ~Dk 15

Hivyo ndivyo unavyoyafikisha maombi yako kwa Mungu kikamilifu. Kwahiyo wewe kama mwana wa Mungu, ukitazingatia kuomba na kutafakari katika hatua hizo, utajikuta muda mrefu upo uweponi mwa Bwana, lakini maombi yako yamejawa na Roho pamoja na bubujiko la ki-Mungu.

Mungu akubariki.

Shalom.

Kwa ushauri/ Msaada/ kuokoka/ Maombezi /Ratiba za ibada, wasiliana nasi kwa mawasilino haya;

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312